Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

Jina la mtahiniwa..... .....

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA
MTIHANI WA MAANDALIZI KABLA YA MTIHANI WA TAIFA
KISWAHILI KIDATO CHA NNE SEPTEMBA 2019

MAELEKEZO: **MUDA SAA 3**

- Karatasi hii ina sehemu A,B, na C zenye jumla ya maswali kumi na mbili (12)
- Jibu maswali yote kutoka Sehemu A na B na chagua maswali matatu kutoka sehemu C
- Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali
- Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
- Andika majina yako ya mtihani katika kila ukurasa

SEHEMU A (Alama 15)
UFAHAMU
Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

1. Wa ubani Rawaziri, na kandoro kadhalika,
   Lumbano la kishairi, gazetini kuliweka,
   Nami nimejikusuri, maoni kuyatamka,
   Ua si ruwaza njema tuzo ya mtu kupewa.

2. Kutunzwa watu wa enzi, kwa ua sijaridhika,
   Siyo zawadi azizi, hasa inoheshimika,
   Bado hamjamaizi, kwa tunzo inosifika,
   Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

3. Ua kupewa harusi, nikaha inapofika,
   Ni siku ya taanusi, kwa bibi kuheshimika,
   Lakini ua si tusi, kwa dume kulipachika,
   Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

4. Ua hupambwa maiti, jeneza likapambika,
   Harufu kila wakati, haiba kuongezeka,
   Na wengine hawataki, uchuro watatamka,
   Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

5. Ua huvishwa mgeni, mtukufu akifika,
   Ni koja la asumini, shingoni linajiweka,
   Mara utalibaini, walinzi wamelishika,
   Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

Jina la mtahiniwa.....

6. Ua tuzo ya mahaba, wapenzi wanahusika,
   Ishara ya usuhuba, wawili kukutanika,
   Lakini na makahaba, na wao hujipachika,
   Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

7. Ua kama lina hadhi, si wote wanaridhika,
   Wengine haliwakidhi, na hata kwa kulishika,
   Sembe kwao ni faradhi, njaa itamwondoka,
   Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

8. Ua likiwa mtini huwa linanawirika,
   Huwa na kubwa thamani, hapo lilipojishika,
   Likitiwa mikononi, si muda linanyauka,
   Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

MASWALI

i) Kichwa cha Shairi hili chaweza kuwa
   a) Ruwaza
   b) Zawadi
   c) Ua si ruwaza njema

ii) Neno " nikaha" kama lilivyotumika katika shairi katika ubeti watatu lina maana ya :
   a) Pingu za maisha
   b) Ndoa
   c) Sherehe ya harusi

iii) Kulingana na shairi hili watu wanaotakiwa kupewa zawadi ya ua ni
   a) Watu wa enzi, wapenzi na maharusi
   b) Maiti, bibi harusi, mgeni na wapenzi
   c) Watu wa aina zote katika shughuli maalum

iv) Ubeti wa saba una maana kwamba
   a) Watu wote hufurahishwa na zawadi ya maua
   b) Zawadi ya maua si utamaduni wa mwafrika hivyo watu wengi hawapendi
   c) Badala ya zawadi ya maua kwa watu wengine ni bora ungewapa chakula.

v) Neno "ruwaza" kama lilivyotumiwa na mwandishi lina maana ya
   a) Zawadi
   b) Nia
   c) Adabu

vi) Mwandishi anaposema "ishara ya usuhuba" ana maana ya
   a) Ishara ya husuda
   b) Alama ya ushirikiano wapenzi wawili
   c) Ishara ya mapenzi

vii) Mawazo makuu ya mwandishi katika shairi lake ni
   a) Zawadi ya maua si nzuri sana kwani ni utamaduni wa kigeni na kiafrika pia.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

Jina la mtahiniwa.....

b) Zawadi ya maua hufaa kwa baadhi ya watu kwa wengine huona kama uchuro.
c) Ua lina hadhi yake lakini si wote wanaopenda zawadi hiyo.

viii) Neno "faradhi" kama lilivyotumiwa na mwandishi lina maana ya
a) Muhimu
b) Fahari
c) Ridhia

ix) Mwandishi katika ubeti wa mwisho anasema kuwa
a) Si vizuri kuyakata maua kutoka mtini
b) Thamani ya ua ni pale linapokuwa mtini kwake
c) Anawalaumu watu wanaoyachuma maua.

x) Mwandishi anaposema " nimejikusuri" anamaanisha
a) Amejikusuru
b) Amejitupa uwanjani
c) Amejizuia

2. Chagua kifungu cha maneno kutoka Orodha B kinachotoa maelezo sahihi ya neno au maneno katika Orodha A kisha andika herufu ya jibu sahihi

ORODHA A	**ORODHA B**
i) Nywa ii) Shamirisho iii) Unyago iv) Mofolojia v) Hatua ya kwanza ya uchanganuzi wa sentensi	A. Ni kielezi au kikundi kielezi kinachotokea upande wa kiarifu B. Neno lenye silabi moja C. Ni nomino au kikundi nomino kinachotokea upande wa kiarifu D. Hupatikana kwenye sarufi maumbo E. Kuainisha maana ya sentensi F. Mzizi G. Kuainisha sentensi H. Sarufi maumbo I. Ni mafunzo ya jadi yatolewayo kwa wanawake kwa lengo la kuwavusha kutoka hatua moja au nyingine J. Ni mafunzo ya jadi yatolewayo kwa watoto wa kike kwa lengo la kuwavusha kutoka hatua ya utoto kwenda ukubwani

SEHEMU B (ALAMA 40)
SARUFI, UTUMIZI WA LUGHA, UANDISHI NA MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. Toa maana nne (04) tofauti za neno "kichwa" kisha tunga sentensi moja kwa kila maana uliyotoa.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

Jina la mtahiniwa.....

4. Kwa kuzingatia mantiki tunga tungo yenye vipashio vifuatavyo na kisha vibainishe vipashio vyenyewe.
Mfano: N+Ts+T+ Ch

Mwanafunzi	alikuwa	anazurura	mtaani
N	Ts	T	ch

a) Nomino +Kishazi tegemezi + Prediketa + shamirisho
b) Kiima kapa +Prediketa + Chagizo
c) Kirai Nomino + Kishazi huru +Kishazi tegemezi
d) W+Ts +T + N

5. "Upatanisho wa kisarufi hufanya nomino mbalimbali kuwa katika kundi moja". Fikiria nomino nane (08) tofauti tofauti na kwa kila nomino tunga sentensi ya umoja na wingi ili kuthibitisha dai hilo huku ukionyesha viambishi vya upatanisho wa kisarufi.

6. "Muundo wa uandishi wa barua za kirafiki na barua za kikazi ni tofauti" Thibitisha kauli hii.

7. Wewe ni mmoja wa wanaharakati wa kutunza mazingira. Andaa risala itakayosomwa siku ya mazingira duniani mwaka 2019. Risala yako isizidi maneno mia mbili (200)

8. "Baada ya Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya Taifa vyombo mbalimbali viliundwa kwa lengo la kukuza na kueneza Kiswahili ,lakini vyombo hivyo hukabiliwa na changamoto mbalimbali" Thibitisha dai hili kwa kutumia hoja nne (04) tu.

SEHEMU C (ALAMA 45)
FASIHI

Jibu maswali matatu (3) katika sehemu hii

9. "Fasihi simulizi imepitwa na wakati kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, hivyo inapaswa kuachwa kutumika katika jamii." Jadili hoja hii kwa kutoa hoja sita.

10. "Nadharia mfumo kike ni jibu faraguzi la mfumo dume katika kazi za fasihi ya Kiswahili". Onesha na eleza jinsi wasanii wa diwani mbili (02) kati ya zilizoorodheshwa walivyoshughulikia suala la mfumo dume katika jamii.

11. Jadili kukubalika kwa wahusika wawili kama kielelezo halisi cha wanajamii kati ya Takadini, Brown Kwacha na Mamantilie kutoka katika riwaya mbili ulizosoma kati ya zilizoorodheshwa.

12. Kwa kutumia tamthiliya mbili (02) kati ya hizo zilizoorodheshwa jadili jinsi kazi za wasanii hao zilivyochangia katika ujenzi wa jamii mpya.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

Jina la mtahiniwa.....

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

Wasakatonge - M.S. Khatibu (DUP)
Malenga wapya – TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka – T.A. Mvungi (EP & D.LTD)

RIWAYA

Takadini – Ben J. Hanson (MBS)
Watoto wa Mama Ntilie – E. Mbogo (H.P)
Joka la Mdimu – A.J. Safari (HP)

TAMTHILIYA

Orodha – Steve Raynolds (MA)
Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe - E. Semzaba (ESC)
Kilio Chetu - Medical Aid Foundation

********MWISHO********

Search ⇢ www.africona.net